

**NAFASI YA TAFSIRI KATIKA TAALUMA YA ONOMASTIKI: UHAKIKI  
WA MBINU ZAKE KATIKA TAFSIRI YA TOPONOMASTIKI**

**BENARD ODOYO OKAL**

[benardodoyo@yahoo.com](mailto:benardodoyo@yahoo.com)

Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika  
Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Kijamii  
Chuo Kikuu cha Maseno  
S.L.P. 333  
MASENO

## **Ikisiri**

Hivi sasa lugha ya Kiswahili inadhukuriwa sio tu kama lugha ya wanajamii wa Afrika Mashariki na Kati pekee bali ni miongoni mwa zile lugha kubwa za ulimwengu na ambazo hutumiwa katika shughuli mbalimbali za binadamu. Hata hivyo, tafiti nyingi zingali zinahitajika ili kukiboresha katika mawasiliano, uwanja wa leksikografia na hata masuala ya tafsiri na onomastiki. Lugha ya Kiswahili inafaa kuchangiwa kwa namna moja au nyingine katika masuala kadha ili iweze kusimama kama lugha inayokua sio katika sarufi peke yake bali pia katika uzalishaji wa taaluma nyingine zinazoweza kufunzwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Taaluma mojawapo ni ile ya tafsiri na onomastiki ambazo sasa zimeanza kukwea milima na kuelekea kudhukuriwa kama taaluma muhimu kwa wanaisimu na hasa wa Kiswahili. Hivyo basi, makala haya yamechunguza nafasi ya taaluma tafsiri na jinsi inavyochangia mafunzo na tafsiri katika taaluma ya onomastiki.

### **1.0 Utangulizi**

Kila kiumbe na hali hupewa majina na binadamu ili kurahisisha mawasiliano na kusaidia katika utambuzi haraka wa kinachozungumziwa. Wanaisimu mbalimbali wanadokeza kuwa neno linalotumiwa kutaja kiumbe au hali aghalabu hudhukuriwa kiisimu kama nomino. Hivyo basi, nomino ni neno linalotumiwa kutaja jina la mahali, mtu, kitu, hali au hata kitendo (TUKI, 2004).

Istilahi nomino linatokana na neno la Kilatini linalojulikana kama ‘nomen’ lenye maana ya neno la kutaja kitu (Habwe & Karanja, 2004). Nomino huwapa watu na vitu vitambulisho na pia ni muhimu katika mawasiliano baina ya watu. Kimsingi nomino ni muhimu katika utambuzi wa kinachorejelewa au kuashiriwa. Kuna aina nyingi za nomino za lugha yoyote ile kama vile nomino za pekee, kawaida, mguso, dhahania, jamii, kitenzi jina na za vitu visivyohesabika (Mgullu, 1999). Mgawanyo huu wa Mgullu ni wa moja kwa moja. Hata hivyo, nomino huweza kugawanywa kwa mujibu wa vigezo kama vile makundi makuu (jumuishi, mahususi, kikundi), makundi madogo (dhahania, mguso, zinazohesabika, zisizohesabika) na kwa kuzingatia vigezo vya kisarufi ambapo pana ngeli za maneno (Kihore, Massamba & Msanjila, 2009). Taaluma inyochunguza majina ya viumbe, hali na kitu chochote huitwa kiisimu kama onomastiki (onomastics) (Crystal, 1987).

Licha ya kuwa kuna aina kadha za nomino, makala haya yanadhamiria kutalii nomino za pekee zinazohusiana na majina ya vitu, viumbe na mahali. Makala yameangazia dhana ya onomastiki kwa ujumla na aina zake, majina ya watu kwa muhtasari na kuhakiki pia mbinu za tafsiri ambazo zimetumiwa katika tafsiri ya majina mbalimbali ya nchi (toponomastiki) ulimwengini kwa kurejelea kongoo katika TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, toleo la pili. Aidha, makala yameshughulikia mbinu mbalimbali za tafsiri na pia uhakiki wa mbinu za tafsiri zilizotumiwa katika tafsiri za majina ya nchi mbalimbali ulimwenguni. Makala haya pia yatakuwa mchango mkubwa katika mafunzo ya taaluma tafsiri inayopendekezwa kama somo kivyake katika mipango ya masomo ya vyuo vikuu mbalimbali.

Makala yametungwa kwa kuzingatia njia ya maktabani ili kujipatia data sekondari faafu ya majina ya nchi mbalimbali ulimwenguni kwa kurejelea *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la pili. Hivyo basi, tumekusanya data za makala haya kwa kutumia sampuli dhamirifu ili kujipatia majina ya nchi yanayopatikana katika kamusi hii na hatimaye kuyachanganua. Makala haya ni muhimu kwa sababu yameshughulikia kwa kina aina mbalimbali za onomastiki na vipera vya aina hizo ili kuwapa wasomaji na watafiti nafasi bora ya kufanya utafiti unaohusiana na taaluma hii ya onomastiki.

## **1.1 Dhana ya Onomastiki**

Onomastiki ni sayansi maalum inayochunguza au kutalii majina ya viumbe (Crystal, 1987). Taaluma hii inajumuisha mbinu za kutambulisha majina ya watu na mahali. Majina ya watu huweza kurejelewa kama anthroponomastiki/anthroponemia (anthroponomastics) inayofupishwa kama anthroponemia (anthroponymy). Kwa upande mwingine, stadi za majina ya mahali hurejelewa kama toponomastiki (toponomastics) ambayo hufupishwa kama toponimia/toponemia (toponymy). Hivyo basi, taaluma ya onomastiki inagawika katika anthroponomastiki inayorejelea majina ya binadamu na pia kuna toponomastiki inayohusiana na majina ya mahali.

### **1.1.1 Anthroponomastiki/anthroponemia**

Aina hii ya onomastiki hutumiwa kwa kurejelea majina ya binadamu. Kuwapa watu majina kunatofautina kutoka lugha moja hadi nyingine na pia kutoka utamaduni

mmoja hadi mwingine. Kila mwanajamii anastahili kuwa na jina maalum. Koigi (2008) anaeleza kuwa kwa mujibu wa Mwalimu Viterlis Wafula Sitati mwandishi wa *Comprehensive Names Dictionary*, majina hufanya jukumu muhimu katika jamii kama vile husaidia katika utambuzi wake kibinafsi na urasmi, kijamii, kiutamaduni na hata kiuchumi. La muhimu ni kuwa kila jina huwa na maana maalum iliyo na thamani yake.

Licha ya kuwa jamii mbalimbali huwa na majina yanayoonekana tofauti kimuundo, kinachodhihirika moja kwa moja ni kuwa jamii hizi mbalimbali huelekea kuwa na mielekeo inayofanana kwa namna mbalimbali ya kupata majina haya. Mwelekeo ni kama vile wa kutazama nyakati za siku, majira, sura au sifa bainifu za mtoto kama vile *Jamila* humaanisha sura nzuri au urembo katika jamii ya waswahili, mfuatano wa kuzaliwa, mfuatano wa majina ya wakwe, matukio mbalimbali na kadhalika. Hivyo basi, majina kwa ujumla hutokana na utamaduni wa mazingira ya jamiilugha husika (Msanjila, Kihore & Massamba, 2009)

Vilevile, majina ya watu huweza kutolewa kwa kurejelea mambo kama vile taaluma au kazi ya mtu, matukio, mahali panapojulikana na kupendeza au hata watu maarufu (Crystal 1987; Mwololo, 2009). Tunaporejelea kazi ya mtu au taaluma yake tunaweza kupata kwa mfano anayeelimisha mara nyingi hurejelewa kama mwalimu huku anayetoa mhadhara huitwa mhadhiri. Majina huweza kutolewa pia kutokana na matukio, mahali panapojulikana na kupendeza, majina ya watu wengine maarufu au kuchukua majina ya watu wenye uhusiano au wa kifamilia, wanyama na kadhalika. Kwa mfano, wanaoitwa *Uhuru* wanaelekea kuzaliwa wakati wa kujinyakulia uhuru kutoka kwa wakoloni.

Aidha, kuna baadhi ya watoto wanaopewa majina kwa kurejelea majina ya watu maarufu ulimwenguni au hata marais kama vile Obama. Kwa mujibu wa Mwololo (2009), ripoti ya *Daily Metro* ya mwishoni mwa mwaka wa 2008 kuhusu watoto waliozaliwa nchini Kenya wakati wa mkesho wa uchaguzi wa Marekani na kuapishwa kwake, inaeleza kuwa baadhi ya wakenya walielekea kuwapa watoto wao waliozaliwa wakati huo majina ya rais Obama au mmoja wa familia yake kama vile Michelle, Malia au Sasha. Ni jambo la kweli kuwa majina ya watu mashuhuri huelekea

kuchukuliwa na watu wengi kama vile katika hospitali ya Pumwani watoto waliozaliwa wengine waliitwa Barrack, Obama au Michelle.

Hali ilikuwa vivyo hivyo katika hospitali kuu ya Mkoa wa Nyanza, ambapo watoto zaidi ya ishirini waliozaliwa waliitwa Obama huku nusu wao kuitwa Michelle. Katika hospitali ya Marie Stopes ya kule Kisumu, takriban watoto kumi waliitwa kama vile *Emmanuel Senator Obama, Brian Obama Otieno, Michelle Akinyi, Walter Barrack* na hata *Michelle Obama*. Ni hakika kuwa sio katika hospitali hizo pekee ambapo wazazi waliamua kuchukua majina kama hayo bali huenda maeneo mengine pia majina kama hayo yalitumiwa kuwaita watoto waliozaliwa wakati huo. Jina hili la rais wa Marekani halikuathiri jamii za kiafrika tu bali lilionekana likiigwa hata kule Marekani kulingana na ripoti ya New York Times.

Majina ya watu huelekea kutumia mikondo anuwai ya ubunifu na hali hiyo huweza kuzalisha dhana zifuatazo katika uchambuzi wa anthroponomastiki kama vile anthroponimu fungwa, anthroponimu siha, anthroponimu za kifamilia, anthroponimu ya kithioforiki, anthroponimu ya kiutani, apotropaiki, matronimu, patronimu, teknonimu, paidinimu, aptronimu na animonimu (Crystal, 1987; Newmark, 1988; Hatch & Brown, 1995; Chebet, 2001; Mwololo, 2009).

#### **i) Anthroponimu fungwa**

Haya ni majina yanayofungamana na mazingira fulani kama vile *Koyo* kumaanisha mazingira ya baridi, *Oyamo* kumaanisha wakati wa upepo mkali na *Akech* ni yule aliyezaliwa katika mazingira ya njaa katika Kiluo. Kwa upande mwingine, *Waweru* ni wa nyikani kwa mujibu wa jamii ya Kikuyu, *Wanjala* ni aliyezaliwa wakati wa njaa na *Nafula* ni aliyezaliwa wakati wa mvua nyingi kwa mujibu wa jamii ya Abaluhya.

#### **ii) Anthroponimu siha**

Haya ni majina ya watoto kama maombezi kwa Mola kama vile *Bahati* na *Baraka* hutumiwa ili kuonyesha kudura ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake.

### iii) Anthroponimu ya kifamilia

Anthroponimu ya kifamilia ni jina linalotumiwa na kila mtu katika familia moja mahususi. Jamii nyingi za kiasia zina mazoea ya kuwa kila mwanafamilia hupewa jina moja la baba ili kujitambulisha na familia hiyo husika. Hata bibi anapoolewa, aghalabu hubadilisha jina lake kwa kuongeza jina la mumuwe ili kujitambulisha na familia hiyo. Mathalani, ikiwa jina la kifamilia ni *Momanyi*, basi watoto wote wa kike au wa kiume huelekea kuchukua jina hili. Kwa hivyo, tunaweza kuwa na *John Momanyi*, *Rachel Momanyi*, *Abdi Momanyi* au hata *Vivian Momanyi*.

### iv) Anthroponimu ya kithioforiki

Mtindo huu hutambua majina ya watu kutokana na masuala ya kidini au kutokana na majina katika Biblia au hata Kurani kama vile *Yohana*, *Luka*, *Musa*, *Abrahamu*, *Rehema* au *Sarah*. Majina haya aghalabu hutolewa kutoka makala ya dini mbalimbali na tunapochunguza majina ya watu wengi, majina haya huchukua nafasi ya kwanza katika mfuatano wa jina la mtu. Kama vile tunaweza kuwa na *Yohana Otieno* au hata *Sarah Nafula*.

### v) Anthroponimu ya kiutani

Anthroponimu ya kiutani hudhukuriwa kama majina ya lakabu ya kumpa mtu kutokana na sifa au hulka au mazoea ya matendo yake au hata pia mafanikio yake katika maisha. Majina kama hayo huweza kutegemea pia mazingira. Mathalani, tunaweza kupata majina ya anthroponimu ya kiutani kama vile *Mzeebia* (anayependa kunywa bia), *Mwanapombe* (anayependa kunywa pombe kwa ujumla), *Mamakelele* (apendaye kupiga kelele) na *Mamantilie* (ni yule mama anayefanya biashara ya kuuza chakula nyumbani au magengeni).

### vi) Apotropaiki

Apotropaiki (apotropaic) ni majina yanayopewa watu ili wasidhurike kutokana na mapepo mabaya dhidi ya binadamu. Aghalabu, majina haya hupewa watoto kama maombezi kwa Maulana ili wasidhurike kutokana na matendo ya mapepo hatari. Kama vile '*Kill Sin*' ni jina la Kipuritani linalotumiwa ili kushtua mapepo mabaya (Crystal, 1987).

### **vii) Teknonimu**

Teknonimu (teknonymy) ni majina ya wazazi yanayoundwa kutokana na majina ya watoto wao (Crystal, 1987). Aina hii ya majina si maarufu sana ulimwenguni hata hivyo hujitokeza mno kule Uarabuni na hata baadhi ya wanajamii wengine wa Kiafrika. Kule Uarabuni, jina la mzazi aghalabu hurejelewa kwa kutumia jina la mwanambee/kifunguakinywa. Mathalani, ikiwa katika familia jina la mwanambee ni Bakari, basi wanajamii watarejelea jina la babake kama *Baba Bakari* au *Mama Bakari* ili kuonyesha heshima fulani katika jamii hiyo husika.

### **viii) Paidinimu**

Paidinimu ni yale majina yanayoundwa kutokana na anthroponimu au majina ya wajukuu. Mathalani, ikiwa jina la mjukuu ni Bakari basi tutakuwa na majina kama vile *Babu Bakari* au hata *Nyanya Bakari*.

### **ix) Animonimu**

Animonimu ni majina yanayotumiwa kuwataja watu mbalimbali hata hivyo majina hayo yanatokana na majina ya wanyama. Mathalani kuna *Little Bear* la Kihindu Marekani (Crystal, 1987), *Buffalo* na hata *Beaver City* (Hatch & Brown, 1995). Katika jamii za kiafrika kuna majina yanayotokana na majina ya wanyama kama vile katika jamii ya waluo, kuna majina ya watu yanayochukua majina ya wanyama kama vile: *Kwach* (chui), *Liech* (ndovu), *Simba* (simba) na hata *Omuga* (Kifaru).

### **x) Aptronimu**

Hii ni istilahi inayotumiwa ili kurejelea majina ya kazi ya mtu na vifaa vilivyoundwa kama vile kuna aptronimu (apronyms) ya kuonyesha majina ya kazi na pia iponimia/iponemia (eponyms) inayoshughulikia majina ya falsafa au vifaa kutokana na majina ya walioviunda. Kuna iponimu zinazotolewa kutoka nomino za kipekee ambapo pana matumizi ya {-ist au -ism} katika lugha ya Kiingereza (Newmark, 1988). Aghalabu, kiambishi tamati {-ist} hutumiwa kuonyesha mtenda kama vile *Marxist* huku {-ism} hutumiwa kurejelea filsofia au falsafa ya mtenda kama vile *Marxism*. Katika lugha ya Kiswahili kiambishi tamati {-ist} katika majina haya ya Kiingereza hutafsiriwa kwa kutumia kiambishi {Ki-} huku nafasi yake ikibadilika na

kuwa kiambishi awali na hatimaye kuunda jina kama vile *Kimaksi*. Kwa upande mwingine, kiambishi tamati {-ism} kinachoonekana katika lugha ya Kiingereza aghalabu hutafsiriwa katika Kiswahili kama kiambishi {U} na hatimaye kuunda majina kama vile *Umaksi*.

#### **xi) Matronimu**

Matronimu (metronymic) ni majina yanayoundwa kutokana na jina la mama au jina la nyanya kwa kujaribu kuongezea sehemu fulani mwanzoni au mwishoni. Kama katika jamii ya wakikuyu nchini Kenya kuna majina kama vile *Waweru wa Wambui* au hata *Samuel Wanjiru*. Majina haya huonyesha kuwa mhusika wa kiume amechukua jina la mama kama ya kifamilia.

#### **xii) Patronimu**

Patronimu (patronymic) ni majina yanayoundwa kutokana na anthroponimu au jina la baba au babu tofauti na majina ya kifamilia. Jamii mbalimbali ulimwenguni huelekea kutumia mitindo anuwai ili kuonyesha kuwa kuna jina la mtu fulani linaloweza kuonyesha moja kwa moja ubashiri wa jina la babake. Yaani, kutokana na jina la mtoto, mtu ambaye hata hajui au kumwona babake mtoto huyo anaweza kuwa na uwezo wa kugundua moja kwa moja jina la babake mhusika fulani. Kuna mitindo mbalimbali inayotumiwa na jamii anuwai kuhusiana na majina ya kipatronimu katika Urusi, Uingereza, Skoti, Ayalandi na hata Polandi (Crystal, 1987). Tazama maelezo yafuatayo:

Kule Urusi, mtoto wa kiume wa *Ivan* ataitwa *Ivanovich* na akiwa mtoto msichana basi ataitwa *Ivanovna*. Kutokana na mifano hii, inabainika kuwa hali ya kiume huonyeshwa kwa kutumia kiambishi tamati {-ovich} na wa kike huwa na kiambishi tamati {-ovna}. Katika lugha ya Kiswahili kunaelekea kuwa mtindo kama huo wa kuongezea kiambishi haufuatwi hata hivyo tunaweza kugundua jina la babake mtoto fulani kwa kutumia maneno maalum kama vile *bin* na *binti*. Hivyo basi tunaweza kuwa na majina kama vile *Hemedi bin Robert*, *Siti binti Saad* au hata *Salome binti Kizito*.



Katika Kiingereza, tunaweza kugundua jina la baba la mtu kutokana na kuongezewa kwa kiambishi tamati {-son}. Mathalani, pana majina kama vile ‘Robertson’ la kuonyesha kuwa anayerejelewa ni mtoto wa kiume wa Robert. Kule Skoti (Scotland) yaonekana kuwa baadhi ya waskoti hutumia kiambishi awali {Mac-/Mc-} pamoja na jina la mzazi ili kujiundia jina linalotakikana. Mathalani tunaweza kuwa na majina kama vile *Mac’Donald* au *Mc’Donald*. Mtindo kama huu huelekea kutumiwa hata na wanajamii mbalimbali barani Afrika sio kulingana na utamaduni wao, bali kwa kuiga mitindo ya wageni. Hivyo basi kuna majina kama *MacOnyango*, *McOnyango*, *MacOgembo*, *McOuma* au hata *McOkal* miongoni mwa wanajamii waluo.

Katika nchi ya Ayalandi, wanaayalandi wana mazoea ya kuongeza kiambishi awali {O’-} pamoja na jina lingine. Hivyo basi, panaweza kutokea kwa majina kama vile *O’Conor* na kadhalika. Katika jamii ya wapolandi kule Polandi, kuna mazoea ya kuongeza kiambishi tamati {-ski} pamoja na majina mengine. Licha ya hayo, wale wanaotoka Welsh wana uzoefu wa kuongeza kiambishi awali {Ap-} ili kujitambulisha.

### **xiii) Anthroponimu kijinsia**

Licha ya kuwa na aina kadha za jinsi tunavyowapa wototo wetu majina kwa mujibu wa kazi, matukio, mahali maarufu, watu maarufu na hata wanyama, kuna pia mtindo wa kurejelea majina hayo ili kutambulisha jinsia ya mtu husika. Hii inamaanisha kuwa kutokana na majina ya watu, tunaweza kugundua kama mtu anayetajwa ni wa kiume au wa kike kwa kutegemea asasi mbalimbali za jamii. Kuna kiambishi kinachotumiwa ama mwanzoni au mwishoni wa jina husika. Mwololo (2009) anaeleza kwa mfano katika jamii ya wakamba kuna *Mwendwa* ambaye ni mtoto wa kiume lenye maana ya kupendwa huku *Mwende* kuwa wa kike wa kupendwa. Kwa kurejelea majina hayo mawili tunaweza kugundua kuwa kuna mabadiliko mwishoni mwa jina ili kuonyesha uana au jinsia kama vile katika *Mwendwa* kuna kiambishi tamati {-wa} huku katika *Mwende* kuna kiambishi tamati {-e}.

Kwa upande mwingine, jamii ya waluo aghalabu huonyesha tofauti kijinsia katika majina kwa kutumia kiambishi awali {O-} kinachotumiwa kuonyesha mtoto wa

kiume au {A-} kuonyesha jinsia ya kike. Matalani kuna *Ochieng'* ambaye ni mtoto wa kiume aliyezaliwa mchana jua likiwaka huku mtoto wa kike aliyezaliwa wakati kama huo huitwa *Achieng'*. Ikiwa ni wakati wa jioni basi mtoto wa kiume ataitwa *Odhiambo* au *Adhiambo* akiwa wa kike. Licha ya kuwa na mitindo ya kuonyesha jinsia ya mtoto katika jina lake, kunaonekana uhuru wakati mwingine kwa sababu unaweza kupata mtoto mvulana katika jamii ya waluo akipewa jina la kike na hali hubadilika hasa tunapoangazia mtoto msichana akipewa jina la jinsia ya kiume kutegemea matakwa ya familia yenyewe kama itikadi yao.

Baada ya kuangazia suala la anthroponomastiki, kuna pia aina nyingine ya onomastiki inayoitwa toponomastiki ambayo kwa hakika ndiyo dhamira ya makala haya. Aina hii ya onomastiki imeangaziwa katika sehemu hii inayofuatia.

### **1.1.2 Toponomastiki/Toponimia**

Hii ni aina ya onomastiki inayochunguza majina mbalimbali yanayorejelea mahali au maeneo. Aghalabu binadamu huweza kupata jina la mazingira yake, taasisi, nchi, nyumba na mahali popote kijiografia. Majina ya mahali huwa na etimolojia au uasili wake kutokana na salua ya jamii husika, imani na hata thamani. Mara nyingi majina ya mahali pa kijiografia huweza kurejelewa kutokana na mambo kama vile ya watu maarufu, wagunduzi au wasafiri, ufalme au ukoo, umuhimu wa kidini, maeneo spesheli, matukio ya maeneo, miji maarufu na pia sura au majina kitoponimu (Crystal, 1987). Kwa mujibu wa Crystal, majina kwa mujibu wa mambo hayo huangaziwa namna hii:

Majina ya watu maarufu kama vile wanasiasa, marais, wasafiri huweza kutumiwa kama majina maalum ya mahali fulani pa kijiografia. Kuna majina kama vile *Delaware*, *Baltimore* na hata *Washington*. Majina ya wagunduzi au wasafiri mbalimbali waliogundua au kufikia eneno fulani pia huonekana tunapotalii suala la toponimia kama vile kuna majina kama *America*, *Cookstown*, *Columbus* na hata *Flinders*. Majina kutokana na ukoo, familia, hadhi na hata ufalme yanaweza kuonekana katika majina ya mahali kama vile *Queensland*, *Victoria Falls*, *New York*, *Maryland*, *Kingston* na pia *Jamaica*.

Kuna vilevile majina ya mahali yanayoonyesha umuhimu wa kidini, kimiungu na kisainti kama vile *Providence*, *Godshill* na *Axminster*. Maeneo spesheli yanayohusiana na labda kambi na ngome/husuni/boma huweza kuonyeshwa kwa mfano *Don Caster* na *Fort Jesus*. Majina mengine ya maeneo huitwa jinsi yalivyo kwa sababu ya matukio yaliyotendeka hapo awali kama vile *Waterloo* na *Manhattan* (pahali pa ulevi wa kupindukia). Miji maarufu hupewa majina ili kuonyesha umaarufu wake kama vile *Paris*, *Memphis* na hata *London*. Katika jamii ya waluo wa Kenya kuna jina la jiji la *Kisumu* kutokana na neno ‘*sumo*’ lenye maana ya hali ya kusaidiana na kuchangiana bidhaa wakati wa njaa.

Mahali pengine hupewa majina kwa kuzingatia sura au topografia yake ambayo inaweza kuwa ya mlima, mabonde, mito, chemchemi na kadhalika. Majina kama yafuatayo huweza kurejelewa kama vile *Dover* (mahali pa maji), *Staines* (mahali pa mawe) na *Honolulu* (mahali salama/bandari salama). Barani Afrika, tuna maeneo kama vile *Dar es Salaam* (Dari salama) ya kule Tanzania na *Bonde la Ufa* la Kenya.

Kila nchi ulimwenguni ina etimolojia yake inayohusiana au kuashiria baadhi ya masuala tuliyoeleza hapo awali. Kimsingi, inadhihirika kuwa majina ya nchi huenda yakibadilika kama tunavyoona katika atlas au ramani za nchi mbalimbali ulimwenguni. Kwa mujibu wa etimolojia ya majina ya nchi mbalimbali ulimwenguni, Crystal (1987) anaangazia majina ya nchi kama haya: *Ajentina* (Argentina) ya Jamhuri ya fedha (The Silver Republic), *Kanari* (Canaries) ya mbwa (Dogs), *Chile* (Chile) yenye maana ya ukingo wa ardhi (End of the land), Saiprasi/Kuproosi ya sehemu ya shaba nyekundu (Copper belt), *Uhabeshi* (Ethiopia) yenye maana ya uso unaochomeka (Burning face), *Jamaika* (Jamaica) penye maji tele (Well watered), *Japani* (Japan) yenye maana ya mzizi wa jua (Sun root) na *Meksiko* (Mexico) ya miungu ya vita (war god). *Pakistani* (Pakistan) ni jina lililoundwa kutokana na akronimu za **P** (unjab) + **A** (fghan) + **K** (ashmir) + **S** (indh) + (Baluchis) **tan**. Crystal (1987) anaendelea kuelezea kuwa majina ya nchi au mahali huelekea kubadilika wakati mwingine kwa kufupishwa. Kuna majina yaliyokuwa marefu na hatimaye kufupishwa kama vile *Los Angeles* ni kifupisho kutokana na ‘*El Pueblo de Nuestra Senora la Reina de los Angeles de Porciun-cula*’ (uk. 115).

Ni jambo lililo gumu kwa watafsiri katika juhudi zao za kutafsiri majina ya watu na hata ya toponimu ya maeneo na nchi. Swali linaloweza kusumbua bongo za wataalamu ni kuwa kuna uwezekano wa kutafsiri majina ya maeneo na nchi mbalimbali? Jibu ni kuwa ni hakika kwamba majina ya nchi mbalimbali huweza kutafsiriwa kutoka lugha moja hadi nyingine. Hivyo basi, ili kujibu swali hili kikamilifu, hatuna budi kuangazia kwanza dhana ya tafsiri na mbinu zake zinazoonekana katika tafsiri ya majina ya nchi anuwai.

## 1.2 Dhana na mbinu za tafsiri

Majina ya nchi, mahali au hata binadamu huweza kutafsiriwa ili kukidhi haja ya watuamijaji wa lugha husika. Hata hivyo, tafsiri inapofanywa shuruti mtafsiri awe amejihami na mbinu kadha za tafsiri na hatimaye kuchuja zile mbinu zinazofaa kutumiwa ili kutafsiri majina kutoka lugha moja hadi nyingine. Tafsiri ni mbinu ya uhamishaji wa ujumbe kutoka lugha moja hadi nyingine (Bright, 1991) na aghalabu husaidia katika urahisishaji wa mawasiliano na uelewano baina ya watu (Crystal, 1987). Uhamishaji unapofanywa kutoka lugha moja hadi nyingine aghalabu nadharia mbili muhimu hurejelewa kama vile nadharia ya ulinganifu/usawazisho au ya kiisimu inayoshughulikia ulinganifu wa ujumbe kwa kuzingatia vipashio vya kiisimu na nadharia ya pili huitwa nadharia uamilifu inayozingatia au kutafsiri ujumbe kwa kulenga nia mahususi ya mawasiliano (Newmark, 1988). Katika nadharia hii ya uamilifu, mtafsiri analazimika kutoa ujumbe wake pasipo kujifunga na kanuni za kisarufi. Kwa ujumla, kuna mbinu mbalimbali za tafsiri kama vile tafsiri neno kwa neno, tafsiri sisisi, ya kiujumisia, ya kiethnografia na hata tafsiri tohozi (Crystal, 1987; Newmark, 1982, 1988; Hatch & Brown, 1995; Kiango, 1995; Mukuthuria, 2007; Oduori, 2008).

Katika tafsiri ya neno kwa neno, mtafsiri anapaswa kutafsiri kutoka lugha moja hadi nyingine kwa kutoa kisawe chake mwafaka kama vile chakula ni *food* katika lugha ya Kiingereza. Tafsiri sisisi ni mbinu inayochunguza miundo ya kiisimu ya lugha asilia na pia ya lugha pokezi ya matini na hatimaye kuhamisha maana ipasavyo. Hii ni kwa sababu, lugha nyingi huwa na miundo tofauti ya mpangilio wa maneno yake. Mathalani, ‘chakula hiki’ huweza kutafsiriwa kama *this food*. Kutokana na mfano

huu, kionyeshi ‘hiki’ katika Kiswahili huja baada ya nomino hali iliyo tofauti tunapotafsiri katika lugha ya Kiingereza ambapo kinakuja kabla ya nomino.

Wakati mwingine tunaweza kurejelea tafsiri ya kiujumisia ili kutafsiri makala ya kisanii kama vile riwaya, tamthilia, hadithi fupi, makala maalum na kadhalika. Umuhimu wake ni kutuletea mhemuko au hisia za kazi husika na pia kutobadilisha mtindo, dhamira, maudhui na matumizi ya lugha ya makala asilia. Tafsiri ya kiethnografia aghalabu hulenga masuala ya kitamaduni ya jamii na lugha yao kwa kuzingatia muktadha na utamaduni.

Kuna pia tafsiri aminifu ya kutafsiri makala kutoka lugha moja hadi nyingine bila ukiushi na hivyo basi hudhihirisha mlingano wa makala asilia na tafsiri katika isimu, maudhui, kiurejelezi na pia mawasiliano. Aina nyingine ya tafsiri ambayo hutumiwa sana na watafsiri katika masuala kadha ambayo huenda hayapatikani katika lugha pokezi ni ile inayoitwa tafsiri tohozi. Tafsiri tohozi inamaanisha mtindo wa kuchukua msamiati wa lugha asilia na kuutafsiri au kuunukuu kwa kufuata kaida za kifonolojia na kimofolojia za lugha pokezi.

Kutafsiri majina ya watu au hata mahali kunaonekana katika makala kadha hata hivyo huwa na changamoto zake kwa sababu mtafsiri anafaa kuangalia kwamba ujumbe wake umewafikia walengwa wake. Hivyo basi ni kazi ngumu kutafsiri majina ya watu na hata maeneo mbalimbali. Kutafsiri majina ya watu huonekana katika kazi za kiufundi za fasihi, vitabu tukufu vya dini na hata vitabu vya leksikografia. Mathalani, katika Nyerere (1969), kuna majina ya wahusika ambayo yametafsiriwa katika lugha ya Kiswahili kama vile *Duke of Venice* (Mtawala wa Venisi), *Prince of Morocco* (Mwana wa Mfalme wa Moroko), *Prince of Arragon* (Mwana wa Mfalme wa Arragoni), *Lorenzo* (Lorenzo), *Shylock* (Shailoki), *Tubal* (Tubali), *Launcelot Gobbo* (Launseloti Gobbo), *Old Gobbo* (Mzee Gobbo), *Leornado* (Leonado), *Balthazar* (Baltazari), *Stephano* (Stephano), *Portia* (Poshia) na *Jessica* (Jessika).

Katika makala ya kidini kama vile Biblia kunaonekana uwezekano wa kutafsiri majina kutoka lugha moja hadi nyingine kama vile kutoka Kiingereza, Kiswahili au hadi Kiluo. Tazama mifano ya baadhi ya vitabu tulivyoteua kutoka Biblia hasa Agano

la Kale kwa mujibu wa International Bible Society (1984) ya Kiingereza, Bible Society of Kenya (1997: v) ya Kiswahili na United Bible Societies (1976: 5) ya Kiluo:

<b>Kiingereza</b>	<b>Kiswahili</b>	<b>Kiluo</b>
Genesis	Mwanzo	Chakruok)
Exodus	Kutoka	Wuok
Leviticus	Mambo ya Walawi	Tim jo-Lawi
Numbers	Hesabu	Kwan
Deuteronomy	Kumbukumbu za Torati	Rapar mar Chik
Job	Ayubu	Ayub
Psalms	Zaburi	Zaburi
Proverbs	Mithali	Ngeche
Ecclesiastes	Mhubiri	Eklesiastes
Lamentations	Maombolezo	Ywagruok

Kutokana na mifano hii miwili kutoka tamthilia ya *Mabepari ya Venisi* na pia *Biblia* ya wakristo, kunabainika bayana kuwa mbinu ya tafsiri tohozi na tafsiri ya neno kwa neno ni muhimu mno katika tafsiri ya onomastiki. Mbinu hizo mbili zimetumika vilevile katika tafsiri ya majina ya nchi mbalimbali katika lugha ya Kiswahili kama tunavyoona katika sehemu hii inayofuatia.

### **1.3 Uhakiki wa mbinu za tafsiri katika tafsiri za nchi mbalimbali**

Nchi mbalimbali ulimwenguni zinaweza kutafsiriwa kutoka lugha moja hadi nyingine kwa kutumia mbinu mbalimbali za tafsiri. Hata hivyo makala haya yanalenga kutazama mbinu zilizotumiwa na wanaleksikografia katika kiambatisho cha TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la pili. Ingawa kuna mbinu kadha za tafsiri, mbinu zote haziwezi kutumiwa katika makala moja na pia katika tafsiri ya majina ya nchi mbalimbali kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili. Baadhi ya mbinu zilizotumiwa na wanaleksikografia katika tafsiri ya nchi mbalimbali mintarafu *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* kutoka Kiingereza hadi Kiswahili ni kama vile tafsiri tohozi, tafsiri sisisi na tafsiri ya neno kwa neno.

#### **1.3.1 Tafsiri tohozi**

Lugha yoyote inapotagusana na nyingine basi aghalabu utohozi wa maneno hutokea ili kukidhia haja ya watu katika mawasiliano. Utohozi ni suala la kiisimujamii na humanisha kuandika neno kwa kufuata kanuni za kifonolojia na komofolojia ya lugha pokezi. Kwa mujibu wa makala haya, tafsiri tohozi imetumika katika tafsiri ya

majina ya nchi mbalimbali ulimwenguni kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili. Mifano ifuatayo huonekana katika nchi za Bara la Afrika:

Algeria (Aljeria), Benin (Benini), Burkinafaso (Bukinafaso), Cameroon (Kameruni), Cape Verde (Kepuvede), Chad (Chadi), Comoros (Komoro), Cote d'Ivoire (Kodivaa), Djibouti (Jibuti), Eritrea (Eritirea), Gabon (Gaboni), Guinea (Gine), Guinea Bissau (Ginebisau), Lesotho (Lesoto), Madagascar (Madagaska), Mauritania (Moritania), Mauritius (Morisi), Morocco (Moroko), Mozambique (Mozambiki/Msumbiji), Niger (Nijeri), Nigeria (Nijeri), Sao Tome and Principe (Saotome na Prinsipe), Senegal (Senegali), Siera Leone (Sieraleone), Sudan (Sudani) na Swaziland (Uswazi).

Katika Bara la Amerika, nchi mbalimbali zimetafsiriwa kwa kutumia mbinu ya utohozi kama vile: Argentina (Ajentina), Bahamas (Bahama), Barbados (Babadosi), Brazil (Brazili), Canada (Kanada), Colombia (Kolombia), Costa Rica (Kostarika), Cuba (Kuba), Dominica (Dominika), Ecuador (Ekwedo), El Salvador (Elsalvado), Georgia (Jojia), Greenland (Grinlandi), Guatemala (Gwatamala), Honduras (Hondurasi), Ikwado (Ekwado), Jamaica (Jamaika), Mexico (Meksiko), Nicaragua (Nikaragwa), Paraguay (Paragwai), Peru (Peruu), Saint Lucia (Santalusia), Saint Vincent and the Grenadines (Santavisenti na Grenadine), Suriname (Surinamu), Trinidad and Tobago (Trinidad na Tobago) na Uruguay (Urugwai).

Katika Bara Asia, nchi zifuatazo zimetafsiriwa kwa kutumia tafsiri tohozi kama vile: Afghanistan (Afuganistani), Azerbaijan (Azabajani), Bahrain (Bahareni), Bangladesh (Bangladeshi), Bhutan (Butani), China (China/Uchina), India (Hindi/India), Iran (Irani), Iraq (Iraki), Japan (Japani), Jordan (Jordani/Yordani), Kampuchea/Cambodia (Kampuchia/Kambodia), Kazakhstan (Kazakistani), Kirgystan (Kirigizitani), Kuwait (Kuwaiti), Lebanon (Lebanoni), Malaysia (Malesia), Maldives (Maldova), Myanmar/Burma (Myama/Bama), Nepal (Nepali), Oman (Omani), Pakistan (Pakistani), Palestine (Palestina), Philippines (Filipino), Qatar (Katari), Singapore (Singapoo/Singapuri), Srilanka (Sirilanka), Syria (Siria), Taiwan (Taiwani), Tajikistan (Tajikistani), Thailand (Tailandi), Turkey (Uturuki), Turkmenistan (Turukimenistani), Uzbekistan (Uzbekistani) na Vietnam (Vietnamu).

Bara la Australesia lililo na nchi chache ulimwenguni pia lina nchi ambayo imetafsiriwa kwa kutumia mbinu ya tafsiri tohozi kama vile New Zealand (Nyuzilandi). Barani Ulaya mna nchi kama vile: Andorra (Andora), Belarus (Belarusi), Belgium (Ubelgiji), Bosnia and Herzegovina (Bosnia na Hazegovina), Britain (Briteni), Croatia (Korasia), Cyprus (Saiprasi/Kuprozi), Denmark (Denmaki), Finland (Ufini), France (Ufaransa), Germany (Ujerumani), Gibraltar (Jibralta), Greece (Ugiriki), Holland/Netherlands (Uholanzi), Hungary (Hungaria), Iceland (Isilandi/Aisilandi), Ireland (Irelandi/Ayalandi), Italy (Italia), Latvia (Lativia), Liechtenstein (Lishenteni), Lithuania (Litwania), Luxembourg (Lasembagi), Macedonia (Masedonia), Norway (Norwe), Poland (Polandi), Spain (Hispania), Sweden (Uswidi/Swideni), Switzerland (Uswizi), Ukraine (Ukraini) na Vatican City (Vatikani).

### **1.3.2 Tafsiri sisisi**

Tafsiri ya nchi nyingine zimefanywa kwa kutoholewa moja kwa moja kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili kulingana na kanuni za kimofolojia na kifonolojia husika. Aidha, wanaleksikografia hawa wametimia mbinu nyingine inayochanganya utohozi na tafsiri sisisi. Tafsiri sisisi inamaanisha uchunguzi wa miundo ya maneno kiisimu kisha kuhamisha maana kwa kufuata kanuni za lugha pokezi. Tafsiri sisisi inahusisha ile hali ya kutafsiri kila neno kwa kufuata mpangilio wa lugha asilia kisha kuyapanga upya kulingana na kanuni za lugha pokezi. Tazama majina ya nchi mbalimbali ambayo yametafsiriwa kwa kuchanganya utohozi na tafsiri sisisi kama vile Barani Afrika, kuna mifano ifuatayo: Central African Republic (Jamhuri ya Afrika ya Kati), Congo Democratic Republic (Kongo Jamhuri ya Kidemokrasia), Congo Republic (Jamhuri ya Kongo), Equatorial Guinea (Ginekweta), South Africa (Afrika Kusini) na Western Sahara (Sahara Magharibi).

Kule Marekani kuna nchi ambazo zimetafsiriwa kwa kutumia tafsiri sisisi kama vile: Caribbean Islands (Visiwa vya Karibiani) na Dominican Republic (Jamhuri ya Dominika). Katika Bara la Asia majina yafuatayo ya nchi mbalimbali yametafsiriwa kwa kuchanganya tafsiri tohozi na tafsiri sisisi kama vile: North Korea Republic (Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu) Kaskazini, Korea (Republic of) South (Korea



Jamhuri ya ) Kusini, Laos (People's Democratic Republic of)-Laosi (Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu), Saudia Arabia (Saudia), United Arab Emirates (Falme za Kiarabu) na Yemen (Arab Republic of)-Yaman (Jamhuri ya Kiarabu ya).

Kule Australesia nchi zifuatazo zimetafsiriwa kwa kutumia utohozi na tafsiri sisisi kama vile: Palau Islands (Palau Visiwa), Papua New Guinea (Papua) na Solomon Islands (Solomoni Visiwani). Bara la Ulaya lina nchi kama vile: Czech (Republic) - Cheki (Jamhuri) na Russia (Federation of) - Urusi (Shirikisho la).

### **1.3.3 Tafsiri ya neno kwa neno**

Tafsiri ya aina hii inapofanywa, basi neno kutoka lugha asilia huweza kupewa kisawe chake mwafaka moja kwa moja katika lugha pokezi. Katika Bara la Afrika, majina ya nchi mbalimbali yametafsiriwa kwa kutumia mbinu hii huku maneno yanayotumiwa kama tafsiri hayana uhusiano moja kwa moja na neno asilia kama vile: Egypt (Misri), Ethiopia (Uhabeshi), Seychelles (Ushelisheli) na Madagascar (Bukini). Katika Bara Amerika, mna nchi kama vile; United States of America (Amerika/Marekani). Kule Ulaya kuna Portugal (Ureno) na United Kingdom (Uingereza).

### **1.4 Ugunduzi**

Inadhihirika bayana kuwa tafsiri tohozi inapotumiwa katika shughuli za kutafsiri makala basi masuala kama yafuatayo ya mofolojia na fonolojia ya lugha asilia na lugha pokezi huzingatiwa. Kwa mujibu wa makala haya kuna:

a) Sauti /g/ katika baadhi ya majina ya nchi kutoka Kiingereza hadi Kiswahili inanukuliwa kama /j/ katika Kiswahili. Hivyo basi, tunapopata majina ya Kiingereza yenye sauti hiyo /g/ hatuna budi kuigeuza hadi sauti /j/ katika Kiswahili kama vile: Algeria (Aljeria), Niger (Nijeri), Nigeria (Nijeria), Argentina (Ajentina), Georgia (Jojia) na Gibraltar (Jibralta).

b) Sauti /c/ inapofuatwa na vokali katika maneno basi aghalabu husikika kama sauti /k/ ikitamkwa. Hali hiyo inaonekana tunapotafsiri kutoka Kiingereza hadi Kiswahili hasa tunapotumia tafsiri tohozi kama vile: Cameroon (Kameruni), Cape Verde

(Kepuvede), Cote D'Ivoire (Kodivaa), Comoros (Komoro), Canada (Kanada), Columbia (Kolombia), Costa Rica (Kostarika) na Cambodia (Kambodia).

c) Sauti /q/ haipo katika uchunguzi wa fonimu za lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo mara nyingi sauti hii hutoholewa kwa kuhamishwa katika Kiswahili kama sauti /k/ na hatimaye kuchangia katika tafsiri ya majina ya nchi kama vile Iraq (Iraki), Qatar (Katari), Equatorial Guinea (Ginekweta) na Mozambique (Mozambiki).

d) Tafsiri tohozi inapotumiwa aghalabu suala la uchunguzi wa silabi hufaa kuzingatiwa. Lugha mbalimbali zina sifa tofauti za kushughulikia silabi zake. Silabi za Kiswahili zinaweza kuchukua miundo ya irabu pekee, konsonanti pekee, konsonanti na irabu na pia konsonanti konsonanti irabu. Hata hivyo kuna aina mbili kuu za silabu za lugha nyingi ulimwenguni kama vile irabu funge inayoishia kwa konsonanti na pia silabi wazi au huru inayoishia kwa irabu (Mgullu, 1999; Habwe & Karanja, 2004). Kwa kuwa kimuundo, lugha ya Kiingereza ni lugha ambishi mchanganyo ambapo maneno yake huambishwa hadi inakuwa vigumu kujua mipaka ya viambishi vyake na lugha ya Kiswahili ni lugha ambishi bainishi ambayo maneno yake huonyesha moja kwa moja mipaka ya viambishi vyake pamoja na silabi zake wazi (Mgullu, 1999), suala la silabi na michakato yake huelekea kutofautiana.

Baadhi ya maneno ya nchi zilizoshughulikiwa huishia kwa konsonanti kwa hivyo yanapotafsiriwa basi suala la silabi za Kiswahili hufaa kutiliwa maanani huku irabu zikilazimishwa kuongezwa mwishoni mwa kila neno linalotoholewa. Mtindo huo huonekana katika takriban majina yote yanayoishia kwa konsonanti. Matalani: Barani Afrika kuna Benin (Benini), Cameroon (Kameruni), Chad (Chadi), Gabon (Gaboni), Niger (Nigeri), Senegal (Senegali) na Sudan (Sudani). Katika Bara la Amerika mna Barbados (Babadosi), Brazil (Brazili) na Greenland (Grinilandi). Katika Bara Asia mna Afghanistan (Afganistani), Bahrain (Bahareni), Bhutan (Butani), Iran (Irani), Japan (Japani) na Jordan (Jordani).

e) Tafsiri tohozi hudhihirisha pia mabadiliko ya kimofonemiki yanayotokea hasa katika uundaji wa maneno ya lugha kwa sababu ya michakato ya kifonolojia ya uburutishaji na usilimishwaji. Mabadiliko ya kimofonemiki hutokea kwamba sauti

/u/+/a/ zikifuatana basi huzalisha sauti kiyeyushi /w/. Hii inamaanisha kuwa iwapo sauti vokali /u/ itafuatwa moja kwa moja na sauti /a/ basi mabadiliko hutokea na kuzalisha sauti /w/. Kama vile katika majina yafuatayo ya nchi mbalimbali: Ecuador (Ikweddo), Guatemala (Gwatamala), Nicaragua (Nikaragwa), Paraguay (Paragwai), Uruguay (Urugwai) na Equatorial Guinea (Ginekweta).

f) Tafsiri tohozi inapotumika basi kunaonekana pia mwambatanisho wa meneno. Maneno ya lugha asilia hutoholewa kwanza na baadaye kuambatanishwa ili kuunda neno moja. Kama vile: Cape Verde (Kepuvede), Cote d'Ivoire (Kodivaa), Equatorial Guinea (Ginekweta), Guine Bissau (Ginebisau), na Sao Tome na Principe (Saotome na Prinsipe). Majina mengine ni kama vile El Salvador (Elsalvado), Saint Vincent na The Grenadines (Santavisenti na Grenadine) na New Zealand (Nyuzilandi).

g) Kuna pia udondoshaji wa maneno au majina tunapotafsiri majina ya nchi kama vile Papua New Guinea (Papua) na Saudia Arabia (Saudia).

## **1.5 Hitimisho**

Tafsiri iliyofanyiwa majina ya nchi anuwai ni faafu huku mbinu za utohozi, tafsiri sisisi na tafsiri ya neno kwa neno zimepewa kipaumbele na wanaleksikografia wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Masuala muhimu ya fonolojia na mofolojia yanayoangaziwa tunapotafsiri kwa kurejelea mbinu hizi yamezingatiwa ipasavyo. Kwa ujumla, makala haya yameshughulikia suala la nomino na aina zake na pia taaluma ya onomastiki inayochunguza majina ya watu, vitu na hata mahali. Aidha, tumeshughulikia aina mbalimbali za onomastiki na mitindo kadha. Mwishoni mwa makala mna uhakiki wa mbinu za tafsiri zilizotumiwa ili kufanikisha tafsiri za majina ya nchi mbalimbali za ulimwengu kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

## **Marejeleo**

Bible Society of Kenya (1997). *Biblia*. Nairobi: Bible Society of Kenya.

Bright, W. (1991). *International Encyclopedia of Linguistics*. London: Oxford University Press.

- Chebet, C. S. (2001). *Anthroponimu Asilia za Kinandi kwa Mtazamo wa Kisemantiki*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Moi, Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika.
- Crystal, D. (1987). *The Cambridge Encyclopedia of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Hatch, E. & Brown, C. (1995). *Vocabulary, Semantics and Language Education*. Cambridge: Cambridge University Press.
- International Bible Society (1984) *The Holy Bible. New International Version*. New Jersey: East Brunswick.
- Kiango, J. G. (1995). Uundaji wa Msamiati Mpya katika Kiswahili. Katika: K. K. Kahigi (mh.) *Kioo cha Lugha*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, uk. 46-54.
- Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B., & Msanjila, Y. P. (2009). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA) Sekondari na Vyu*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Koigi, J. (2008, Machi 1). Literary Scene: What is in a name? Katika: *Daily Nation*. Nairobi: Nation Media Group, uk. 37.
- Mgullu, S. R. (1999). *Mtalaa wa Isimu*. Nairobi: Longhorn.
- Msanjila, Y. P., Kihore, Y. M., & Massamba, D. P. B. (2009). *Isimujamii Sekondari na Vyu*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mukuthuria, M. (2007). Mchango wa Tafsiri katika Tanzu za Kitaaluma za Kiswahili. Katika: K. Njogu (mh.) *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya*. Nairobi: Twaweza Communications & CHAKITA, uk.119-134.
- Mwololo, M. (2009, Januari 28). Living Magazine: What do you call your child? Katika: *Daily Nation*. Nairobi: Nation Media Group, uk.6-7.
- Newmark, P. (1982). *Approaches to Translation*. New York: Prentice Hall International.
- \_\_\_\_\_. (1988). *A Textbook of Translation*. New York: Prentice Hall International.
- Nyerere, J. K. (1969). *Mabepari wa Venisi*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Oduori, W. R. (2008). Uchunguzi wa Nadharia za Tafsiri: Mwelekeo wa Usemezano. Katika: N. O. Ogechi, N. L. Shitemi & K. I. Simala (wh.) *Nadharia katika*

*Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.* Chuo Kikuu cha Moi: Moi University Press, uk. 333-41.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la Pili.* Dar es Salaam: TUKI.

United Bible Societies (1976). *Muma Maler.* Nairobi: The Bible Society of Kenya.